



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za

Usafiri Ardhini



Tarehe: 21 Septemba, 2026

TANGAZO LA NAFASI ZA KUWA MJUMBE WA KAMATI ZA WATUMIAJI WA HUDUMA ZA USAFIRI ARDHINI MIKOA (RCC)

{Mikoa ya: Shinyanga, Geita & Simiyu}

KIPINDI CHA MAOMBI: Jumatano Tarehe 23/09/2026 Hadi Ijumaa, Tarehe 02/10/2026

Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA Consumer Consultative Council, LATRA CCC), lipo kwa mujibu wa Kif. Namba 29 cha Sheria Namba 3 ya Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini, (LATRA) ya Mwaka 2019 na Marejeo yake ya mwaka 2025.

1.0 MAJUKUMU YA BARAZA:

Baraza lina Majukumu yafuatayo:

- (i) Kuwakilisha maslahi ya watumiaji wa huduma za usafiri kwa njia ya Reli, usafiri wa umma kwa njia ya barabara, usafiri wa chini ya ardhi na usafiri kwa njia ya waya, kwa kuwasilisha, kupata maoni na taarifa na kwa kushauriana na Mamlaka, Waziri mwenye dhamana na wadau wa sekta mbalimbali zinazodhibitiwa;
- (ii) Kupokea na kusambaza taarifa na maoni mbalimbali kuhusu masuala yanayowagusa watumiaji wa huduma zinazosimamiwa na LATRA;
- (iii) Kuunda kamati za Watumiaji wa huduma za usafiri wa Sekta zinazodhibitiwa na LATRA katika Mikoa na Kushauriana nazo;
- (iv) Kushauriana na wadau, Serikali na makundi ya watumiaji kuhusu huduma;
- (v) Kuunda majukwaa kwenye maeneo ya shule/vyuo/taasisi zenye Watumiaji wa huduma za usafiri wa Sekta zinazodhibitiwa na Kushauriana nazo;
- (vi) Kufanya utafiti juu ya maslahi, haki, wajibu na masuala mengine yanayogusa watumiaji.

Katika kutekeleza jukumu la 1.0 (iii) hapo juu, Baraza llinatangaza nafasi tano (05) za Wajumbe wa Kamati ya Watumiaji Huduma za Usafiri Ardhini (RCC) katika Mkoa tajwa hapo juu.

2.0 MAJUKUMU YA KAMATI (RCC):

Kamati za Mikoa za Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (RCC) zina majukumu yafuatayo:

- (i) Kushauriana na Baraza kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu maslahi ya watumiaji wa huduma zinazodhibitiwa ndani ya mkoa.*
- (ii) Kupokea, kukusanya na kusambaza taarifa pamoja na maoni kuhusu masuala yanayohusu maslahi ya watumiaji wa huduma zinazodhibitiwa ndani ya mkoa.*
- (iii) Kusaidia watumiaji katika mkoa kuhusu masuala yanayohusu maslahi yao na kuendeleza utetezi wa haki za watumiaji katika ngazi ya mkoa.*
- (iv) Kuanzisha, kuratibu na kusimamia vilabu vya watumiaji mashuleni pamoja na majukwaa ya watumiaji ndani ya mkoa.*
- (v) Kufanya vikao na kupitisha maazimio kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu maslahi ya watumiaji ndani ya mkoa.*
- (vi) Kusaidia Baraza katika kuandaa na kutekeleza kampeni za uelimishaji na uhamasishaji wa watumiaji ndani ya mkoa.*
- (vii) Kufanya tafiti na ukusanyaji wa taarifa kuhusu masuala yanayoathiri maslahi ya watumiaji wa huduma zinazodhibitiwa ndani ya mkoa, na kuwasilisha mapendekezo kwa Baraza.*

3.0 SIFA ZA MWOMBAJI:

- (i) Awe Mtanzania, mwenye akili timamu, mchapa kazi na mwenye umri kuanzia miaka 18 na kuendelea*
- (ii) Asiwe mmiliki wa chombo chochote cha kutoa huduma ya usafiri wa Ardhini.*
- (iii) Awe anaishi au ni mwajiriwa-mkazi ndani ya mkoa husika*
- (iv) Awe mwenye nguvu, moyo na nafasi ya kujitolea kufanya kazi na kujituma kwa ajili ya kuisaidia jamii juu ya masuala yanayohusu usafiri ardhini.*
- (v) Awe anajua kusoma na kuandika lugha ya Kiswahili na uwezo wa kuwasiliana na watu*
- (vi) Awe mzalendo na mwaminifu kwa mali na rasilimali za umma.*
- (vii) Wanawake wanahimizwa kuomba.*

4.0 UTARATIBU:

Mtu yeyote mwenye sifa tajwa hapo juu atume maombi yake kwa anuani au barua pepe ya Baraza akiambatanisha: wasifu wake (CV), Vivuli vya vyeti vya Elimu, Picha ya hivi karibuni (passport size) ndani ya siku kumi (10) tangu tarehe ya tangazo hili.

NB: Andika namba yako ya simu inayopatikana kwa ajili ya mawasiliano na Baraza.

5.0 MASLAHI:

Nafasi hii ya Ujumbe wa Kamati ya Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini Mkoa (RCC) ni ya kujitolea na si nafasi ya Ajira.

Tuma maombi kwa:

*Katibu Mtendaji,
Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za
Usafiri Ardhini,
Jengo la Wizara ya Elimu, Magogoni, ghorofa ya 1
Chumba Na. 107,
Mtaa wa Magogoni,
S.L.P 14154,
Dar es Salaam.*

Barua pepe: barua@latracco.go.tz